**SEHEMU YA KWANZA :LUGHA**

***SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI***

1. Umepewa kijikaratasi hiki cha maswali na karatasi ya majibu. Kijikaratasi hiki kina maswali 50.
2. Katika karatasi ya majibu hakikisha umeandika:

   *(i) Jina lako* *(ii) Jina la shule yako*

***Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua kiteuzi kifaacho zaidi.***

Mtoto ni ____1____hasa ____2____ na binadamu. Kiumbe ____3____ huwa ni zawadi ya ____4____ kutoka ____5____Mungu. Kwa ____6____wakati ____7____ huitwa malaika hasa akiwa mchanga. Hivyo basi____8____ ana jukumu kubwa la kumlea mtoto vizuri. Malezi mema yanahusu kumpa mwana chakula____9____, malazi____10____,makazi elimu na vilevile mashauri yafaayo.

Akilini mwanafunzi ____11____ maarifa na bidii. Huamka asubuhi kuandaa staftahi na kujitayarisha kwenda____12____. Hufika skulini ____13____ gwaride. Baadaye hupanga vitabu na madaftari____14____ tayari ____15____ masomo.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. jiumbe | B. kiumbe | C.mvumba | D. liumbe |
| 2. | A.anayezaliwa | B.anaozaliwa | C.anaozalia | D.anaowazalia |
| 3. | A.hawa | B.hao | C.huyu | D.hicho |
| 4. | A.dhamiri | B.dhamana | C.thamani | D.dhamani |
| 5. | A.kwa | B.na | C.ya | D.wa |
| 6. | A.hivyo | B.hivi | C.hivio | D.ivio |
| 7. | A.ingine | B.mwingine | C.mwingineo | D.nyingine |
| 8. | A.kizazi | B.msasi | C.mzazi | D.mzaa |
| 9. | A.boresha | B.kiboresha | C.bibora | D.bora |
| 10. | A.mzuri | B.mazuri | C.nzuri | D.manzuri |
| 11. | A.mwenye | B.wenye | C.yenye | D.lenye |
| 12. | A.shule | B.mashule | C.shuleni | D.mashuleni |
| 13. | A.kati ya | B.kando ya | C.nyuma ya | D.kabla ya |
| 14. | A.mwake | B.yake | C.zake | D.wake |
| 15. | A.kuanza | B. kwanza | C.kuanzia | D.kuanzisha |

***Kuanzia swali la 16-30, kulingana na maagizo***

16. **Teua jibu sahihi**

    ***Jiko____tulitumia kupika ni kubwa.***

    A. ambayo B. ambako

    C. ambao D ambalo

17. Umoja wa ndevu ni;

    A. mandevu B. kidevu

    C. ndevu D. udevu

18. Mkufu ni pambo linalovaliwa kwenye

    A. shingo B. kiwiko

    C. pua D. mguu

19. Kitanda ambacho wagonjwa hubebwa nacho hospitalini huitwaje?

    A. matakia B. plasta

    C.machela D. chimbuko

20. Ni sentensi ipi kati ya hizi iliyo katika hali ya mazoea

    A. yeye aliamka asubuhi sana

    B. yeye ameamka asubuhi sana

    C. yeye anaamka asubuhi sana

    D. yeye huamka asubuhi sana

21. Akisami $^1/_7$ ni

    A. theluthi B. subui

    C. sudusu D. thumni

22. **Kanusha sentensi ifuatayo**

    ***Ataandika insha fupi***

    A. Hataandika insha fupi

    B. Hawataandika insha fupi

    C. Hamtaandika insha fupi

    D. Hatutaandika insha fupi

23. ***Tegua kitendawili hiki***

    ***Hushiriki kuandaa chakula ila hali***

    A. nyuki B. moyo

    C. kitanda D. sufuria

24. Ng'ombe wetu____maziwa mengi.

    A. hukamliwa B. ukamiwa

    C. hukamwa D. ukamliwa

25. ***Anayevumilia shida mwishowe hufaulu.***

    Ni methali gani hudhihirisha maelezo haya?

    A. Adhabu ya kaburi aijuaye ni maiti.

    B. Mstahimilivu hula mbivu.

    C. Chema chajiuza kibaya chajitembeza.

    D. Ajizi ni nyumba ya njaa.

26. ***Tumia kiulizi -ipi kwa usahihi***

    ***Maji yalimiminwa katika ndoo______?***

    A. upi B. ipi

    C. lipi D. yapi

27. ***Kamilisha tashbihi ifuatayo***

    ***Msiri kama___________***

    A. kobe B. twiga

    C. simba D. kaburi

28. ***Tumia 'amba' kikamilifu***

    ***Mchungwa_____umekauka umekatwa***

    A. ambao B. ambayo

    C. ambacho D. ambamo

29. ***Andika sentensi hii kwa wingi***

    ***Jina refu liliandikwa vibaya***

    A. Jina ndefu yaliandikwa vibaya.

    B. Jina ndefu liliandikwa vibaya.

    C. Majina marefu yaliandikwa vibaya.

    D. Majina marefu ziliandikwa vibaya.

30. ***Geuza kwa udogo***

    ***Mji wetu ni mdogo***

    A. kijiji chetu ni mdogo

    B. Kimji chetu ni kidogo

    C. Kijiji yetu ni kidogo

    D. Kijiji chetu ni kidogo

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali ya 31 - 40.***

Hivi majuzi, yaani Jumamosi iliyopita, nilikata shauri kuabiri gari ili kwenda kumzuru shangazi yangu ambaye sikuwa nimemwona kwa mwezi na dahari. Shangazi alikuwa akiishi mtaa wa Talia, umbali wa kilomita kumi na tano hivi upande wa mashariki ya jiji nilimoishi.

Naam, matatu ilikuwa imejaa sisisi abiria ambao pengine walikuwa wametoka kazini kurejea kwao kuburudika baada ya wiki nzima ya kuraukia kazi. Ndani kulikuwa na joto kama tanuri lakini nilivumilia tu ilimradi nifike mapema. Barabara hiyo haikuwa na magari mengi ya abiria. Punde si punde, dereva barobaro alichupia gari na kulitia ufunguo.

Sisi haoo! Baada ya kulipa jiji kisogo, tulikuwa barasteni safari imeiva. Mara, msadidii wa dereva alininyoshea mkono akidai haki yake. Bila wasiwasi wala wahaka, niliupeleka mkono mfukoni ili kumtolea haki yake. Masalaale! Moyo ulianza kunienda mbio nilipokosa hela mfukoni! wacha kijasho chembamba kinitunge kipajini na kibaridi kunivaa vaa! Nilijaribu kuongea lakini hata sauti ilinifeli.

**31.** Msimulizi alienda kumtembelea shangazi yake siku ya.
A. Majuzi B. Jumamosi
C. Jumapili D. Alhamisi

**32.** Shangazi ni?
A. dada yake mama B. ndugu ya kike
C. dada yake baba D. jirani wa mtu

**33.** Msimulizi alisafiri kwa
A. matatu B. miguu
C. meli D. ndege

**34.** Pesa za usafiri garini huitwa
A. Ada B. Kiingilio
C. Nauli D. Kivusho

**35.** Shangazi wa msimulizi aliishi katika mtaa ulioitwa
A. Tala B. Dahari
C. Kwao D. Talia

**36.** Ndani ya matatu kulikuwa na nini?
A. maji B. joto
C. fahali D. mbuzi

**37.** Shangazi aliishi upande wa ______ ya jiji.
A. Mashariki
B. kaskazini
C. magharibi
D. kusini

**38.** Msaidizi wa dereva katika gari ya abiria huitwa
A. Utingo
B. Mpagazi
C. Dalali
D. Dereva mdogo

**39.** Msimulizi alipopeleka mkono mfukoni
A. alipata pesa
B. alipata nyoka
C. alikosa pesa
D. aliumwa

**40.** Kichwa mwafaka cha habari hii kinastahili kuwa
A. shangazi
B. safari
C. kuibiwa na mwizi
D. safari ambayo sitasahau

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali ya 41 - 50.***

Jina langu ni Salama. Nasoma darala la tano. Katika shule ya msingi ya malezi. Mama yangu ni mjasirimali anayefanya biashara ya kuuza mitumba katika soko la Kariokoo. Baba yangu ni kandawala wa kutoka Mombasa hadi Nairobi. N. wapongeza wazazi wangu kwa kunilea nikiwa mwenye afya njema. Yote hayo ni kutokana na kupewa chakula chenye lishe kamili.

Kila asubuhi mama huniandalia uji mtamu wa mtama na maziwa kabla ya kwenda shuleni. Mchana, kishuka changu huwa sima kwa mchicha; mboga zilizo tamu sana. Wakati wa usiku hula wali kwa nyama au chakula kingine kulingana na maandalizi ya mamangu.

Kwa kweli sina tabia ya kula ovyo, kwani baba na mama hunikataza. Mtu alaye ovyo huwa mlafi kama fisi na mwenye tamaa sana. Ukila ovyo unaweza kupata maradhi mabaya au tumbo litashindwa kusaga chakula kutokana na wingi wa chakula tumboni. Nawaomba wazazi wetu watupe chakula kulingana na mahitaji ya kukua kwetu. Hata tukiwa shuleni, walimu hutueleza kuhusu umuhimu wa kuwa na mlo kamili.

Napata uchungu kuona watoto wengine wakikosa chakula bora huku wengine wakitupa vyakula mapipani badala ya kuwapa wenzetu wasiokuwa na chochote. Naomba serikali kuituma misaada ya chakula kwenye sehemu zisizo na vyakula vya kutosha kuliwa. Swali ni je, bila chakula miili yetu ingekuwa vipi?

**41.** Ni kweli kusema kwamba:

A. Baba yake mwandishi ni mfanyabiashara mashuhuri

B. Mama yake mwandishi huitwa salama

C. Baba yake mwandishi ni kandawala

D. Familia ya mwandishi huishi kwa njaa sana

**42.** Salama ni mtoto ____ vizuri na kuwa mwenye afya nzuri.

A. aliyelewa B. aliyelelewa
C. aliyelewalewa D. aliyeula

**43.** Chakula cha mchana huitwa chamcha au ________

A. kishuka B. staftahi
C. chajio D. kisebeho

**44.** Chagua sentensi isiyo na makosa

A. mama huniandalia uji tamu

B. ukila ovyo unaweza kupata magonjwa mbaya

C. chakula mbovu hutupwa

D. watoto wasile chakula kingi

**45.** Ni mnyama yupi hula sana kulingana na ufahamu?

A. salama B. paka
C. mbwa D. fisi

**46.** Chakula cha asubuhi huitwa

A. staftahi B. kishuka
C. chajio D. kisebeho

**47.** Jina mtoto liko katika ngeli gani?

A. KI-VI B. LI - YA
C. A - WA D. YA - YA

**48.** Watoto hupewa chakula ili_____vizuri.

A. wakuwe B. wakue
C. wakuliwe D. waliwe

**49.** Mahindi, mchele,maharagwe, wimbi na mtama, kwa jumla huitwa

A. sima B. kidona
C. pure D. nafaka

**50.** Ni tabia ipi ambayo haimpendezi mwandishi?

A. Ulafi

B. Ulevi

C. Kukula chakula chenye lishe kamili

D. Kula chakula shuleni